**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**



# MWONGOZO WA UUNDAJI NA URATIBU WA JUKWAA LA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

**JANUARI, 2025**

## YALIYOMO

**VIFUPISHO VYA MANENO ........................................................................ iii**

**FASILI YA MANENO ........................................................................ iv**

**TAMKO LA WAZIRI ........................................................................ vii**

**DIBAJI ........................................................................ viii**

**SHUKRANI ........................................................................ x**

**SURA YA KWANZA ........................................................................ 1**

**1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1**

1.2 Chimbuko la Jukwaa ........................................................................ 2

1.2 Malengo ya Mwongozo ........................................................................ 3

1.5 Hatua za uandaaji wa Mwongozo ........................................................................ 3

1.6 Mapitio ya Mwongozo (2022). ........................................................................ 4

**SURA YA PILI ........................................................................ 5**

**2.0 JUHUDI ZA KIMKAKATI ZA SERIKALI NA MIFUMO YA KISERA KUHUSU UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........................................................................ 5**

2.2 Mifumo ya Kisera Kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ........................................................................ 6

**SURA YA TATU ........................................................................ 10**

**3.0 UUNDAJI NA MUUNDO WA JUKWAA ........................................................................ 10**

3.0.1 Jukwaa la Mtaa/ Kijiji ........................................................................ 11

3.0.4 Jukwaa la Mkoa ........................................................................ 12

3.2 Muundo wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ........................................................................ 13

**SURA YA NNE ........................................................................ 14**

**4.0 UONGOZI NA UENDESHAJI WA JUKWAA ........................................................................ 14**

4.0 Uongozi ........................................................................ 14

4.0.1 Sifa za Viongozi ........................................................................ 14

4.0.2 Majukumu ya Viongozi ........................................................................ 14

4.0.3 Muda wa Uongozi na Ukomo wa Uongozi ........................................................................ 16

4.0.3.2 Kusitishwa kwa Kiongozi ........................................................................ 16

4.1 Uendeshaji wa Jukwaa ........................................................................ 17

4.2 Mikutano ya Jukwaa ........................................................................ 17

4.2.1 Jukwaa la Mtaa/Kijiji ........................................................................ 17

4.2.2 Jukwaa ngazi la Kata ........................................................................ 17

4.2.3 Jukwaa ngazi la Wilaya ........ 18
4.2.4 Jukwaa ngazi la Mkoa ........ 18
**SURA YA TANO ........ 20**
**5.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU ........ 20**
5.0 Ofisi ya Rais - Ikulu ........ 20
5.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI ........ 20
5.2 OR –Mipango na Uwezeshaji ........ 21
5.3 Ofisi ya Waziri Mkuu ........ 21
5.4 Wizara ya Fedha ........ 22
5.5 Kamati ya Uongozi ........ 22
5.6 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum . 22
5.7 Wizara za Kisekta ........ 23
5.8 Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC). ........ 23
5.9 Sekretarieti ........ 24
5.10 Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 24
5.10.1 Sekretariati za Mikoa ........ 24
5.10.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 25
5.13 Ofisi ya Kata ........ 26
5.14 Ofisi ya Mtaa/ Kijiji ........ 26
**SURA YA SITA ........ 27**
**6.0 UTARATIBU WA KUGHARAMIA SHUGHULI ZA JUKWAA ........ 27**
6.0 Vyanzo Vya Mapato ya Jukwaa ***........ 27***
**SURA YA SABA ........ 28**
**7.0 UFUATILIAJI NA TATHIMINI ........ 28**
7.1. Ufuatiliaji ........ 28
7.2 Tathmini ........ 29
7.3 Utoaji wa Taarifa za utekelezaji ........ 30
**SURA YA NANE ........ 31**
**8.0 HITIMISHO ........ 31**

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| CFGs | - | *Community Financial Groups* |
| NEEC | - | *National Economic Empowerment Council* |
| OWM | - | *Ofisi ya Waziri Mkuu* |
| SMEs | - | *Small Medium Entreprises* |
| WDF | - | *Women Development Fund* |
| SDGs | - | *Sustainable Development Goals* |
| TWCC | - | *Tanzania Women Chamber of Commerce* |
| SIDO | - | *Small Industries Development Organisation* |
| UN | - | *United Nations* |
| GEF | - | *Generation Equality Forum* |
| WMJJWM | - | *Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum* |
| OR-TAMISEMI | - | *Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa* |
| MSM | - | *Mamlaka ya Serikali za Mitaa* |
| | - | *Ofisi ya Rais Mipango na Uwezeshaji* |

## FASILI YA MANENO

| | |
|---|---|
| **Uwezeshaji wanawake** | Ni juhudi zinazofanywa na Serikali kuwapa wanawake elimu na mbinu mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. |
| **Uwezeshaji kiuchumi** | Ni juhudi za makusudi zinazotekelezwa na Serikali na wadau kwa lengo la kukuza na kuongeza maarifa, ujuzi, uwezo wa kiuchumi na fedha kwa Wananchi ili kuwasaidia kushiriki shughuli za Maendeleo. |
| **Shughuli za kiuchumi** | Ni shughuli ambazo zinafanywa na mtu binafsi, shirika au taasisi kwa lengo la kuwezesha kiuchumi mtu binafsi, vikundi vya watu, vyama au kampuni ili kutengeneza kipato kupitia kilimo, biashara, uchimbaji madini, usafirishaji, utalii, uzalishaji, ujenzi, utoaji uvuvi, ufugaji na huduma. |
| **Mifuko ya uwezeshaji** | Ni mifuko inayotoa huduma mbalimbali kwa wananchi hususani vijana, wanawake ikiwemo mikopo, dhamana na ruzuku ili kuwawezesha wananchi kuanzisha na kupanua shughuli za kiuchumi pamoja na kuinua hali zao za maisha. |
| **Misaada/Mikopo** | Ni kitu au fedha yoyote inatolewa na wadau mbalimbali wakiwemo washirika wa maendeleo yenye riba na isiyo na riba, makampuni na asasi za kiraia kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma. |

| | |
|---|---|
| **Mapato** | Ni fedha yoyote ambayo inaingia katika mifuko na programu kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo ruzuku kutoka Serikali Kuu na misaada kutoka kwa wadau pamoja na riba inayotokana na mikopo, tozo mbalimbali au ushuru. |
| **Vihatarishi** | Ni viashiria vinavyosababishwa na udhaifu wa ndani au nguvu ya nje ambazo zinaweza kutokea na kuathiri utendaji wa Jukwaa la Uwezeshaji |

| | |
|---|---|
| **Jukwa la Wanawake** | Utaratibu unaowawezesha wanawake kukaa pamoja ili kujadiliana na kupeana taarifa kuhusu fursa mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa zilizopo na changamoto zinazowakabili na kuja na utatuzi wa changamoto hizo. |
| **Mwanamke** | Ni mjasriamali aliye mwanachama wa kikundi kilichosajiliwa na mamlaka husika mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea. |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | Ni muundo wa utawala unaohusisha kukasimisha madaraka ya utawala kwa wananchi kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Halmashauri. |
| **Jinsia** | Mgawanyo wa majukumu baina ya wanawake na wanaume katika jamii. Mgawanyo huo unatokana na mitizamo iliyojengeka ndani ya jamii husika ambapo majukumu hayo yanaweza kutofautiana kulingana na muda au jamii moja na nyingine. |
| **Ukatili wa Kijinsia** | Ni kitendo chochote anachofanyiwa mwanamke au mwanaume kinachoweza kusababisha madhara ya kimwili, kiakili, kisaikolojia, kiuchumi au mateso mengine. |
| **Ukatili wa kiuchumi** | Ni hali ya kutokuwa na sauti katika mali inayokuhusu, kufanyishwa kazi kwa malipo kidogo, kutomiliki mali inayokuhusu, usafirishwaji wa wanawake na wasichana. |
| **Umasikini** | Hali ya kushindwa kumudu mahitaji ya kimsingi Viashiria |

## TAMKO LA WAZIRI

Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikitekeleza jukumu la kuwezesha Wanawake Kiuchumi hapa nchini ili kuwa na uwezeshaji wenye ufanisi na unaohakikisha mwanamke anashiriki shughuli za kiuchumi na kumiliki rasilimali, kila kiongozi hana budi kuhakikisha kuwa rasilimali za Serikali na uwekezaji unaofanyika unaleta tija kwa wanawake na Taifa kwa ujumla. Dhamira hii itawezekana tu pale ambapo viongozi watafuatilia uwekezaji unaofanyika katika maeneo yao ya kiutendaji na kupata taarifa ambazo zitaisaidia Serikali kupima kama uwekezaji huo unaleta ustawi na maendeleo ya wanawake na Taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto ya Wanawake kupata taarifa muhimu kuhusu shughuli zao kiuchumi na pia kupata taarifa za utekelezaji wa shughuli zinazofanyika katika kuwawezesha wanawake kijamii, kisiasa na kiuchumi. Uundaji na uratibu wa mwongozo huu wa Jukwaa la Uwezeshaji wanawake kiuchumi unaweka misingi ya utekelezaji wa majukumu ya Jukwaa ili kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao na kuchochea mchango wao katika ujenzi wa taifa.

Serikali imeandaa mwongozo unaolenga kuhakikisha kuwa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, yanaanzishwa na kuimarishwa nchini ili yaweze kuwasaidia wanawake waliopo kwenye vikundi vya maendeleo vya kiuchumi kutoka katika sekta mbalimbali za uzalishaji pamoja na wanawake walioko kwenye tasnia ya Sanaa na Michezo ambao watatumika kama hamasa katika uundwaji wa vikundi na kujikwamua kiuchumi. Rai yangu ni kuona kuwa, kila mdau aliyeainishwa katika Mwongozo huu anatekeleza majukumu yake ili kufikia malengo ya uundaji na uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

Hivyo, ninatoa wito kwa Wizara za Kisekta, Idara za Serikali zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau kwa ujumla kutumia Mwongozo huu katika kutekeleza masuala yote ya uwezeshaji wanawake kiuchumi hapa nchini.

Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM.**

## DIBAJI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linapongeza hatua iliyochukuliwa ya kuandaa mwongozo huu ambao ni nyenzo kubwa na ya muhimu katika kufanikisha uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Serikali yetu imedhamiria kuwainua wanawake ili kuleta maendeleo ya haraka kwenye nchi yetu. Kama sote tunavyofahamu wanawake ni kundi muhimu sana katika Jamii yetu na mchango wao unaleta matokeo ya haraka kwenye uchumi wa nchi yetu.

Utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unategemea sana ushiriki wa wanawake ambao ni wengi kwa idadi ikilinganishwa na wanaume, na mchango wao ni mkubwa katika kutengeneza Jamii bora. **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Wizara ya kimkakati na yenye dhamana ya wanawake na vilevile inahusika katika kuleta maendeleo ya wanawake katika nyanja zote.** Wizara hii imekuwa na mchango mkubwa sana kwa wanawake kwa kuweka mazingira ya kisera na programu mbalimbali za kuleta maendeleo ya wanawake.

Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kufanikisha mpango wa kuwaleta wanawake pamoja kwa maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii. **Huu ndio mpango pekee ambao unawakutanisha wanawake kwa ajili ya kuzungumzia shughuli zao za maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa. Pia ni fursa ya wao kujua jinsi ya kutatua changamoto zao.**

Uundaji na Uratibu wa Jukwaa ni muhimu katika **kuwezesha wanawake kupata taarifa, kujengewa uwezo, kuongezewa ujuzi, kuunganishwa na fursa mbalimbali, kuunganishwa na wanawake wenzao ili kuleta ufanisi wa shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.** Utengenezwaji wa mfumo huu wa jukwaa unakuwa ni daraja la kuleta mafanikio kwa wanawake kwa kuwa ni namna ya **urasimishaji wa mtandao wa wanawake**. Vilevile ni rahisi kwa Serikali kupanga na kutekeleza mpango wowote wa maendeleo kupitia jukwaa.

Shime kwetu sote ambao tunafanya kazi katika kusaidia kuleta maendeleo ya wanawake, tuzingatie na tuutumie mwongozo huu ili tuweze kufanikisha azma ya Serikali yetu. Wizara zote, Mikoa yote, Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali,

Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi zisaidie katika kutekeleza Mwongozo huu.

Beng'i M. Issa

**KATIBU MTENDAJI**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

## SHUKRANI

Mwongozo huu wa Uundaji na Uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ni matokeo ya jitihada za pamoja kati ya Serikali na Wadau mbalimbali wanaozingatia kipaumbele cha uwepo na utekelezaji wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi zote.

Wizara kwa namna ya pekee, inatoa shukrani za dhati kwa, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Chama cha Wafanya Biashara Wanawake Tanzania (TWCC) na ULINGO kwa kushiriki kikamilifu katika uandaaji wa Mwongozo huu ambao utawezesha Wanawake kuwa na jukumu la pamoja la kujua fursa na utatuzi wa changamoto zao.

Aidha, shukrani za kipekee ziwaendee Wakuu wa Taasisi na Mashirika mbalimbali kwa kuteua na kuruhusu wataalamu wao kushiriki katika mchakato wa uandaaji wa Mwongozo huu wakiwemo watendaji wa Wizara yenye dhamana na Wanawake hapa nchini.

Dkt. John A.K Jingu

**KATIBU MKUU WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Matokeo ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaonesha kuwa asilimia 51 ya watanzania wote ni Wanawake na hivyo kuthibitisha umuhimu wao katika maendeleo ya Taifa letu. Hata hivyo, kutokana na sababu za kihistoria, wanawake bado wamekuwa katika nafasi za chini kijamii na kiuchumi jambo ambalo ndio msingi wa kuanzisha mkakati huu wa Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Licha ya wanawake kuwa ni asilimia kubwa ya nguvu kazi inayotegemewa na Taifa, lakini wamekuwa na umiliki mdogo wa rasilimali ama kutumia mapato yatokanayo na shughuli zao ambapo kwa asilimia kubwa huchukuliwa na kumilikiwa na wanaume. Kwa wanawake wanaofanya biashara ndogondogo, changamoto kubwa ni mitaji midogo isiyojitosheleza, matumizi ya nyenzo duni, ujuzi mdogo, masoko kwa bidhaa zao, mila kandamizi na kukosa dhamana ambayo inaweza kuwasaidia kupata mikopo ili kuongeza mitaji yao Ili kuondokana na changamoto hizo.

Serikali imefanya jitihada mbalimbali za kisera na mifumo zilizowezesha maendeleo ya wanawake, mfano kutungwa kwa Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2000 na mapitio yake ya mwaka 2023 ambayo kwa sasa inaitwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023, Maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), Kuundwa kwa Wizara mahsusi ya kushughulikia masuala ya Wanawake, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF), uanzishwaji wa Mpango wa kukopesha Wanawake mikopo isiyokuwa na riba kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri, uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake ambayo kwa sasa imeunganishwa na Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB) na kuanzishwa madirisha mahsusi ya kuhudumia Wanawake katika baadhi ya Benki kama NMB, CRDB, Equity, Azania na benki nyinginezo.

Uundaji na Uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi ni mwendelezo wa juhudi za Serikali za kuhakikisha watanzania wote wanashiriki sawa katika harakati za maendeleo hapa nchini ikiwa ni utekelezaji wa moja ya makubaliano ya Kimataifa. Jukwaa hili linategemewa kuwa kiungo cha kuwajengea uwezo wanawake ili waweze kuondokana na vikwazo vya kihistoria na kitamaduni ambavyo vinawaweka katika nafasi ya kutofaidika na rasilimali za nchi. Aidha, Jukwaa litasaidia kuongeza uelewa wa wanawake katika nyanja zote.

Katika kutekeleza mwongozo huu, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeandaa

Mwongozo wa Kitaifa wa Uundaji na Uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi Toleo la Mwaka 2024.

### 1.2 Chimbuko la Jukwaa

Malengo 17 ya Milenia ya mwaka 2000, hususan lengo Namba 5 limetaja na kuelekeza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kama nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo ya haraka. Katika kusaidia kufikia malengo ya maendeleo endelevu, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Ban Ki-moon aliteua jopo la viongozi mwaka 2016 ili kumshauri kuhusu njia bora ya kupunguza na kuondoa tofauti iliyojengeka kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchumi Duniani. Halikadhalika kwa lengo la kufikia malengo ya maendeleo endelevu pamoja na uwiano wa 50/50 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye wakati huo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa mmoja wa wajumbe wa jopo hilo. Katika kufanikisha malengo ya kukuza ushiriki na uwezeshaji kiuchumi kwa Wanawake, Mheshimiwa Rais (Wakati huo akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) alizindua rasmi Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi mnamo tarehe 6 Juni 2016. Aidha, katika uzinduzi huo, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliagiza uandaliwe mkakati wa kuanzishwa kwa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi hapa nchini.

Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na wadau lilitengeneza Hadidu za Rejea, muundo na kazi za Jukwaa la wanawake pamoja na maelekezo ya uanzishwaji wa Jukwaa hilo yalipelekwa Mikoa yote kwa Waraka wa Mwezi Disemba, 2016. Baraza lilitoa Waraka huu kwa Makatibu Tawala wote wa Mikoa na kuelekeza kufanyika kwa uanzishaji na uzinduzi wa Jukwaa la wanawake kupitia Madawati ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na kubuni programu mbalimbali za uwezeshaji wanawake kiuchumi. Maelekezo yalikuwa kwamba Mikoa yote iwe imeanzisha Jukwaa la awali kabla ya tarehe 31 Machi 2017. Hadi kufikia Machi 2023, Mikoa 26 ilifanikiwa kuanzisha Majukwaa ya kuwawezesha wanawake kiuchumi.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

### 1.2.1 Lengo Kuu

Kuhakikisha kuwa uundaji na uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi nchini unafanyika kwa ufanisi.

### 1.2.2 Malengo mahsusi ya Mwongozo

i. Kuweka utaratibu wa kuunda, kuendesha na kuboresha Jukwaa la uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Mkoa, Wilaya, Kata, na Vijiji/Mtaa);
ii. Kuainisha majukumu na usimamizi wa Jukwaa kwa kila ngazi;
iii. Kuainisha taratibu za uundaji, uratibu, uendeshaji na utawala wa Jukwaa;

## 1.3 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo utakuza uelewa kuhusu Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na taratibu za uundaji na uratibu wake. Pia, utawezesha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Jukwaa hapa nchini.

## 1.4 Walengwa na Watumiaji wa Mwongozo

Mwongozo huu ni wanawake walio kwenye vikundi kutoka katika sekta mbalimbali za uzalishaji wakiwemo wanawake wenye ulemavu na wanawake walio katika tasnia ya sanaa na michezo kwa ajili ya kuunda Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Aidha, watumiaji wa Mwongozo ni pamoja na Wizara za uratibu (WMJJWM, OR-TAMISEMI, OWM, Wizara ya Fedha, na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi), Wizara za Kisekta, Taasisi zenye dhamana ya Uwezeshaji Wanawake kiuchumi, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo na Asasi za Kiraia.

## 1.5 Hatua za uandaaji wa Mwongozo

Mwongozo huu katika uandaaji wake ulihusisha hatua zifuatazo:

i. Kuundwa kwa Timu iliyojumuisha Wataalamu kutoka OR-TAMISEMI, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania na Taasisi ya ULINGO;
ii. Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wa Mwaka 2022;
iii. Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Uundaji na Uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (Toleo la Pili)
iv. Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Mwongozo.

## 1.6 Mapitio ya Mwongozo (2022).

Kwa kuzingatia msingi wa kuanzishwa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Serikali imefanya mapitio ya Mwongozo wa Mwaka 2022 yaliyogusa maeneo makuu mawili ambayo ni uanzishwaji na uendeshaji wa Jukwaa la Uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa ngazi zote ili kuja na maeneo mapya ya uundaji na uratibu ambayo ndiyo msingi katika Mwongozo wa sasa. Katika eneo la uundaji, Mwongozo umeainisha jukwaa kuwa litaundwa na vikundi vya wanawake wajasiriamali kutoka katika sekta mbalimbali za uzalishaji wakiwemo wanawake wenye ulemavu na walio kwenye tasnia ya sanaa na michezo. Kwa upande wa uratibu ni kuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wameongezwa kuwa walezi wa majukwaa haya. Vilevile Mabadiliko ya msingi yaliyofanyika kwenye Mwongozo tofauti na wa awali ni kuanzishwa kwa Sekrtetariati ya Kitaifa ya Jukwaa ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia, kuratibu na kufuatilia utendaji wa majukwaa nchini na kuondolewa kwa jukwaa la Kitaifa ambapo kwa sasa uundaji wa jukwaa utaishia ngazi ya Mkoa.

## SURA YA PILI

### 2.0 JUHUDI ZA KIMKAKATI ZA SERIKALI NA MIFUMO YA KISERA KUHUSU UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### 2.1 Juhudi za Serikali kuwezesha Wanawake.

Kwa mujibu wa Tathmini ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) imeonesha kuwa, katika kipindi cha miaka ishirini (20) iliyopita, mafanikio kadhaa yamekuwepo katika kuanzisha mifumo inayowezesha wanawake kiuchumi. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na utoaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 743.7 ambazo zimetolewa kupitia Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambapo jumla ya walengwa 6,064,957 wamenufaika na mikopo hiyo; kati yao wanawake ni 3,288,186 sawa na asilimia 54 na wanaume 2,776,771, sawa na asilimia 46 kupitia mifuko mbalimbali ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi likiwemo dirisha la Wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania; kuanzishwa kwa Vitambulisho vya Machinga wakiwemo wanawake vilivyowezesha uhuru kwa wajasiriamali wadogo kufanya biashara ambapo wajasiriamali 441,163 walinufaika na vitambulisho hivyo Kadhalika, kuboresha utendaji wa sekta ya fedha hasa kulenga kuwafikia walengwa wengi katika mazingira ya vijijini pia imekuwa ni kipaumbele muhimu cha utendaji. Serikali kupitia Mifuko 72 ambayo ipo katika Wizara mbalimbali na Taasisi za Serikali na Binafsi imekuwa ikitoa Mikopo ya moja kwa moja, Dhamana, Ruzuku pamoja na Programu za Uwezeshaji ambazo kwa ujumla wake hadi kufikia Machi, 2023, mifuko hii imeweza kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Trilioni 6.1 kwa wajasiriamali 8,650,257 wakiwemo wanawake 4,747,321 na wanaume 3,902,936. Aidha, mifuko na programu hizi zimetengeneza jumla ya ajira 17,603,271 ambapo ajira kwa wanawake zilikuwa 9,248,916 (52.5%) na ajira kwa wanaume ni 8,354,355 (47.5%).

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha (2020/21 - 2029/30), zipo Taasisi 65 za benki na fedha zikiwemo benki za biashara (38), benki za jamii (6), Taasisi za fedha za maendeleo (2), benki ndogo za fedha (5), mikopo ya nyumba (2), makampuni ya kukodisha ya kifedha

(3) na ofisi ya kumbukumbu ya mikopo (20). Aidha, Benki za biashara kama Benki ya NMB, CRDB Bank Ltd na Akiba Commercial Bank (ACB) wameanzisha huduma za masoko ya fedha katika maeneo ya vijijini. Hii imeongeza kiasi cha mikopo ya mtu mmoja mmoja kutoka Shilingi bilioni 1,745.00 mwaka 2013 hadi shilingi bilioni 23,432.80 mwaka 2019.

Serikali imetekeleza azma yake ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba yenye maslahi kwa vikundi vya Wanawake (4%), Vijana (4%) na Watu wenye Ulemavu (2%). Jumla ya Tsh. bilioni 79.16 ilitolewa kwa vikundi 30,041 vya wanawake vinavyojumuisha wanawake 942,110 katika Halmashauri kufikia kwa mwaka 2022/23.

Juhudi zimefanyika kuanzishwa kwa vikundi vya Akiba na Mikopo na Vyama vya Ushirika kusaidia watu ambao hawana sifa ya kupata mikopo kutoka Taasisi za fedha ili kukuza mitaji yao kwa kuweka akiba na kukopa. Pia, Serikali ilijitahidi kuwawezesha wanawake kutatua changamoto za biashara za wajasiriamali ambapo jumla ya hekta 15,822.64 zilitengwa kama maeneo ya biashara katika Halmashauri 150. Aidha, Serikali iliondoa takriban kodi 108, ada na tozo za biashara kati ya 139 ili kupunguza vikwazo vya kodi na kujenga mazingira wezeshi ya biashara. Ukuzaji wa bidhaa za wanawake wajasiriamali katika soko la ndani na nje kwa kuhimiza wanawake kushiriki katika maonesho ya biashara ya kitaifa na kimataifa kama vile Sabasaba, Nanenane na Juakali iliongeza idadi ya wanawake wanaoshiriki katika maonesho ya biashara kutoka 268 mwaka 2010 hadi wanawake 13,566 mwaka 2020. Mafanikio mengine ni pamoja na kuunda Mfumo wa Ujumuishaji wa Kifedha II (2018 - 2022) ambao unatoa kipaumbele katika kushughulikia suala la uwezeshwaji wanawake kifedha.

## 2.2 Mifumo ya Kisera Kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Uandaaji wa Mwongozo huu umezingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho ya mara kwa mara, Sera, Sheria, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, Mipango, Mikakati na maelekezo ya Serikali ambayo yamewezesha uzingatiaji wa mwongozo wa Jukwaa kama ifuatavyo:

A. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka

1977(kama ilivyofanyiwa mapitio ya mara kwa mara) ibara ya 4. Sehemu ya 1 kifungu na. 33 kinatoa uhuru wa mtu kujumuika na kushirikiana na wengine; kifungu na. 34 kinatoa uhuru wa kushiriki shughuli za umma; kifungu na. 35 kinatoa haki ya kila mtu kufanya kazi; na kifungu na. 47 kifungu kidogo cha (2), kinazitaka mamlaka za nchi kuweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia masuala yanayohusu utekelezaji wa masharti ya ibara hii ikiwa ni pamoja na kukuza utu, heshima, usalama na fursa za wanawake wakiwemo wajane;

B. Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 na Mkakati wake wa Utekelezaji wa mwaka 2023 katika eneo la kuinua vipato vya wanawake na kuwajengea uwezo wa kushiriki na kupunguza umaskini;

C. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo inatoa mwongozo wa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeandaliwa kwa kuzingatia nguzo tisa (9) ambazo zitawezesha watanzania kumiliki uchumi wa Nchi. Nguzo hizo ni: (a) Uboreshaji wa mfumo wa utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma nyingine za serikali; (b) Kukuza mitaji; (c) Kukuza uchumi wa mazingira bora ya uwekezaji; (d) Matumizi bora ya ardhi; (e) Uimarishaji wa masoko na ubia; (f) Wananchi kunufaika na ubinafsishaji na hisa; (g) Miundombinu ya kiuchumi; (h) Kuinua viwango vya elimu na ujuzi na (i) Kuimarisha ushirika nchini;

D. Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025 ibara ya 231 (f) kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazotolewa na wanawake wajasiriamali kupitia maonesho ya biashara ya ndani na nje;

E. Mwitikio wa kuhakikisha malengo ya maendeleo endelevu yanafikiwa na malengo ya 50 kwa 50 ya dunia kufikia mwaka 2030. Jukumu kubwa likiwa ni kutathmini shughuli

za uwezeshaji wanawake duniani na kuweka mikakati ya kuongeza fursa za wanawake katika shughuli za kiuchumi na kuhakikisha kuwa Usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi unafikiwa ifikapo mwaka 2030 (SDGs Goal 5);

F. Maelekezo ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suhuhu Hassan (6 Juni, 2016) ambapo alisisitiza kuanzishwa kwa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika mikoa yote ya Tanzania Bara, na 08 Juni, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiongea katika Mkutano na Wanawake wote nchini kupitia wanawake wa Mkoa wa Dodoma, aliagiza kuimarisha Majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili kutoa mchango katika maendeleo ya wanawake na kukuza pato la Taifa;

G. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III Sehemu ya pili) ambapo mfumo wa utendaji wa TASAF umezingatia uwakilishi wa mwanamke. Kwa hiyo mfuko huu umekuwa msaada mkubwa kwa wanawake ili kutokomeza umaskini wa kipato kwa kaya maskini hususani wanawake walio kwenye mpango;

H. Sera ya Huduma ndogo za Kifedha ya mwaka 2017 na sheria ya huduma ndogo za kifedha ya mwaka 2018 zimewezesha mwanamke kujikwamua kwenye umaskini wa kipato kwa kushiriki katika vikundi vya kiuchumi na vikundi vya VICOBA ambapo wanawake wengi wanajiunga katika vikundi hivyo ambapo usajili kwa mujibu wa sheria hiyo ya huduma ndogo za fedha imesaidia na kufanya kuwa kinga kwa wanawake;

I. Dira ya maendelo ya taifa ya 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), kwa pamoja vinasisitiza “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu wakiwemo

wanawake ili kuondokana na umaskini wa kipato;

J. Malengo ya maendeleo endelevu SDG Ajenda hiyo yenye malengo 17 ya maendeleo endelevu yanalenga pamoja na mambo mengine kutokomeza umaskini uliokithiri, kupambana na tofauti na ukosefu wa haki na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, jukwaa hili litatoa nafasi kwa mwanamke kuona fursa na changamoto katika kupambana na umaskini wa kipato miongoni mwao.

# SURA YA TATU

## 3.0 UUNDAJI NA MUUNDO WA JUKWAA

Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ni fursa ya kuwakutanisha Wanawake ili waweze kujadili masuala ya maendeleo ikiwemo biashara, kilimo, mifugo, uvuvi, madini, ujenzi, uchukuzi, elimu, uraia, maadili, malezi, mabadiliko ya tabianchi, ushiriki katika shughuli za kisiasa, Sanaa, teknolojia, michezo na shughuli nyingine za kimaendeleo. Majukumu ya Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ni:

i. Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya kiuchumi vya wanawake;
ii. Kuwaunganisha Wanawake wajasiriamali na fursa za masoko na mitaji;
iii. Kuwezesha Wanawake kujadili kwa pamoja shughuli zao za kiuchumi ikijumuisha biashara, kilimo, madini, ujenzi, siasa, Sanaa, teknolojia, michezo, elimu na uraia pamoja na masuala mengine ya kimaendeleo;
iv. Kubadili mtazamo hasi na kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi;
v. Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia sahihi na rahisi kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji;
vi. Kuwaunganisha na kuwakutanisha wanawake wajasiriamali na watoa huduma katika sekta za Umma na Binafsi;
vii. Kuwajengea uwezo wanawake katika umiliki wa ardhi, mirathi na masuala ya maendeleo kama vile utunzaji wa kumbukumbu, urasimishaji wa biashara, elimu ya kodi, ufungashaji bidhaa, maandiko ya miradi n.k;
viii. Kuhamasisha Wanawake kuhusu elimu ya uraia, uzalendo, maadili na kuendeleza Tunu za Taifa;
ix. Kuwajengea uwezo Wanawake ili waweze kuondokana na tamaduni na mila zenye madhara.

## 3.0 Muundo wa Jukwaa

Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi litafuata hatua zifuatazo kuanzia ngazi ya msingi ya Mtaa/Kijiji, Kata, Wilaya hadi Mkoa. Aidha, utaratibu wa kuzingatiwa katika kila ngazi ni kama ifuatavyo:

### 3.0.1 Jukwaa la Mtaa/ Kijiji

Jukwaa la ngazi ya Mtaa/Kijiji litaundwa na vikundi vya wanawake kutoka katika sekta mbalimbali za kiuchumi **vilivyosajiliwa** katika ngazi husika kwa utaratibu ufuatao:

i. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji wataratibu zoezi la **utambuzi wa vikundi** vya Wanawake vilivyopo katika Mtaa/Kijiji;

ii. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata atahamasisha Wanawake waliopo katika ngazi husika kuhusu uundaji wa Jukwaa la Mtaa/Kijiji kwa Wanawake waliopo katika vikundi;

iii. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata kwa kushirikina na Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji wataorodhesha vikundi vilivyotayari kwa ajili ya kuunda jukwaa. Mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa uorodheshaji wa vikundi hivyo ni pamoja na: Jina la kikundi, namba ya usajili, mahali kilipo, idadi ya wanachama, viongozi wake na mawasiliano yao. (Kiambatisho Na 1: Rejista ya kuandikisha vikundi);

iv. Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji wataitisha mkutano kwa tarehe iliyopangwa utakaohusisha wanawake wote waliopo katika vikundi vilivyoorodheshwa kwa ajili ya kuunda Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi la Mtaa/Kijiji. Katika mkutano huo watachagua viongozi wa Jukwaa lao. Viongozi watakaochaguliwa ni Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Mtunza Hazina. Aidha, Mkutano utachagua Wajumbe watano kutoka miongoni mwao ambao watawawakilisha katika Jukwaa la Kata;

v. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata atasimamia uchaguzi huo na atatakiwa kuhakikisha Viongozi watakaochaguliwa wasitoke katika kikundi kimoja;

vi. Jukwaa litaanzishwa na vikundi vilivyopo kwenye Mtaa /Kijiji na vinavyotambuliwa na vilivyosajiliwa na mamlaka husika.

### 3.0.2 Jukwaa la Kata.

Jukwaa la ngazi ya Kata litaundwa na wawakilishi 10 kutoka Jukwaa la kila Mtaa/Kijiji ambao ni viongozi 5 na Wawakilishi 5 aliochaguliwa katika Jukwaa la ngazi ya Mtaa/Kijiji. Jukwaa la Kata litaundwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:

i. Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata kwa kushirikina na Afisa Mtendaji Kata wataitisha Mkutano kwa tarehe iliyopangwa kwa ajili ya kuunda Jukwaa la Kata la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi;
ii. Baada ya uhamasishaji, kutaendeshwa uchaguzi wa viongozi wa Jukwaa la Kata ambao ni Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti, Katibu, Katibu msaidizi wanaotokana na kundi la wajumbe watano viongozi ngazi ya Mtaa/Kijiji;
iii. Aidha, Mkutano pia utachagua wawakilishi 3 kutoka miongoni mwa wajumbe kuwakilisha Kata katika Jukwaa la Wilaya;
iv. Uchaguzi huu utasimamiwa na Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri ambae pia atahakikisha Viongozi watakaochaguliwa wasitoke katika Mtaa/Kijiji kimoja.

### 3.0.3 Jukwaa la Wilaya

Jukwaa la ngazi ya Wilaya litaundwa na wawakilishi 5 ambao ni viongozi 2 (Mwenyekiti na Katibu wa Jukwaa la Kata) na Wawakilishi 3 waliochaguliwa katika Jukwaa la Kata. Jukwaa la Wilaya litaundwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:

i. Mkurugenzi wa Halmashauri husika kwa kuzingatia mwongozo, ataitisha Mkutano kwa tarehe iliyopangwa kwa ajili kuunda Jukwaa la Wilaya la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi;
ii. Katibu Tawala wa Wilaya husika atasimamia uchaguzi wa viongozi wa Jukwaa la Wilaya ambao ni Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti, Katibu na Katibu Msaidizi;
iii. Aidha, Mkutano pia utachagua wawakilishi 2 kutoka miongoni mwa wajumbe kundi la wawakilishi kutoka ngazi ya Wilaya kuwakilisha Wilaya katika Jukwaa la Mkoa;
iv. Katibu Tawala wa Wilaya husika pia atahakikisha Viongozi watakaochaguliwa wasitoke katika Kata moja;
v. Kwa Wilaya zenye Halmashauri zaidi ya moja uwakilishi utoke kwenye kila Halmashauri na kila Mkurugenzi wa Halmashauri atawajibika katika usimamizi na utekelezaji wa jukwaa katika Halmashauri yake.

### 3.0.4 Jukwaa la Mkoa


Jukwaa la ngazi ya Mkoa litaundwa na wawakilishi 4 ambao ni viongozi 2

(Mwenyekiti na Katibu wa Jukwaa la Wilaya) na Wawakilishi 2 waliochaguliwa katika Jukwaa la Wilaya. Jukwaa la Mkoa litaundwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:

i. Katibu Tawala wa Mkoa kwa kuzingatia mwongozo, ataitisha Mkutano kwa tarehe iliyopangwa kwa ajili kuunda Jukwaa la Mkoa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi;
ii. Katibu Tawala wa Mkoa husika atasimamia uchaguzi wa viongozi wa Jukwaa la Mkoa ambao ni Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti, Katibu na Katibu Msaidizi. Pia atahakikisha Viongozi watakaochaguliwa wasitoke katika Wilaya moja.

### 3.2 Muundo wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

**Jedwali: Na. 1: Chati ya Muundo wa Jukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**




*Chanzo**: Mwongozo wa Uuundaji na uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.***

## SURA YA NNE

### 4.0 UONGOZI NA UENDESHAJI WA JUKWAA

Mwongozo umeainisha nafasi za uongozi, sifa, wajibu na majukumu ya Viongozi, muda na ukomo wa uongozi na uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi mbalimbali.

### 4.0 Uongozi

Uongozi wa jukwaa utakuwa na viongozi wanne (4) isipokuwa Jukwaa la Mtaa/Kijiji ambalo litakuwa na viongozi watano (5) kama ifuatavyo:

i. Mwenyekiti;
ii. Makamu Mwenyekiti;
iii. Katibu;
iv. Katibu Msaidizi;
v. Mweka Hazina (Kwa ngazi ya Mtaa/Kijiji tu).

### 4.0.1 Sifa za Viongozi

Viongozi wa Jukwaa katika ngazi zote wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

i. Awe ana umri wa zaidi ya miaka kumi na nane (18);
ii. Awe Mtanzania;
iii. Awe na akili timamu;
iv. Awe anajua kusoma na kuandika;
v. Awe mwanachama wa kikundi/chama/shirikisho/mjasiriamali kutoka kwenye eneo husika;
vi. Asiwe kiongozi wa chama chochote cha siasa katika eneo husika;
vii. Awe na uelewa kuhusu masuala ya ujasiriamali ;
viii. Awe na utashi wa kujikwamua kiuchumi;
ix. Asiwe amewahi kukutwa na makosa ya Jinai;
x. Awe mwadilifu, mchapakazi, mwenye kujiheshimu na kuheshimu wenzake;
xi. Awe na ari ya kujitolea katika kutekeleza majukumu ya Jukwaa;
xii. Awe mbunifu katika kutafuta fursa za fedha na kuongeza mapato katika Jukwaa.

### 4.0.2 Majukumu ya Viongozi

i. **Mwenyekiti wa Jukwaa:**

a) Kuitisha Mkutano Mkuu wa Jukwaa na mikutano ya dharura;

b) Atakuwa ni msemaji mkuu wa Jukwaa;
c) Ni kiongozi/msimamizi wa shughuli zote za Jukwaa;
d) Atahakikisha jukwaa linaimarika na kusimamia mwongozo kikamilifu
e) Ni mwenyekiti wa vikao vyote vya Jukwaa;
f) Kukaimisha majukumu yake kwa makamu Mwenyekiti endapo hatakuwepo.

ii. **Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa:**

Atakaimu na kutekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti endapo mwenyekiti hatakuwepo.

**NB:** *Makamu Mwenyekiti atatekeleza majukumu atakayoelekezwa na Mwenyekiti*

**(iii) Katibu wa Jukwaa:**

(i) Ni Mtendaji Mkuu wa Jukwaa;

(ii) Ni mwandishi na mtunza kumbukumbu za vikao vyote vya Jukwaa;

(iii) Ni mtayarishaji wa taratibu zote za vikao vya Jukwaa kwa kushirikiana na mwenyekiti;

(iv) Mfuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio na mipango ya Jukwaa;

(v) Mwandishi mkuu wa mawasiliano na taarifa nyingine.

**(iv) Katibu Msaidizi wa Jukwaa:**

Ni msaidizi wa Katibu kwa majukumu yote atakayopewa na Katibu na kukaimu nafasi ya katibu endapo hatakuwepo.

**(v) Mweka Hazina wa Jukwaa la Mtaa/Kijiji:**

(i) Mtunzaji fedha na mtoa taarifa ya mapato na matumizi ya Jukwaa;

(ii) Ni mtoaji wa taarifa zote zinazohusu mapato na matumizi ya Jukwaa;

(iii) Ni mtengenezaji/muandaaji wa bajeti ya Jukwaa;

(iv) Mtunzaji wa Rasilimali za Jukwaa.

**NB**. Mtunza hazina angalau awe na uelewa wa shughuli za kutunza

fedha na atakuwa katika ngazi ya Kijiji/mtaa

### 4.0.3 Muda wa Uongozi na Ukomo wa Uongozi

#### 4.0.3.1 Muda wa Uongozi katika Jukwaa

(i) Muda wa uongozi katika Jukwaa utakuwa ni miaka mitatu (3) ;

(ii) Viongozi waliomaliza muda wao wanaweza kuchaguliwa lakini wasiwe wameshikilia nafasi hiyo kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo.

#### 4.0.3.2 Kusitishwa kwa Kiongozi

Kiongozi anaweza kusitishwa wakati wowote kabla ya muda wa uongozi kuisha endapo:

(i) Hatowajibika ipasavyo katika kuleta maendeleo ya jukwaa kwa mujibu wa uongozi;

(ii) Wanachama wakikosa imani naye kwa idadi ya theluthi mbili ya wanachama wote;

(iii) Ataamua kujiuzulu kwa ridhaa yake mwenyewe kwa maslahi ya jukwaa;

(iv) Iwapo atakosa uaminifu katika mali za jukwaa, atatumia kauli na lugha isiyokuwa na staha kwa wanachama na jamii;

(v) Iwapo atakuwa amefariki au kuhama Mtaa/Kijiji, Kata, Wilaya na Mkoa;

(vi) Iwapo atakuwa amekosa uwezo wa kutimiza wajibu wake kutokana na sababu za Kiafya au sababu zingine zozote zilizothubitishwa na wanachama.

**Tanbihi:** Kiongozi aliyemaliza muda wake atalazimika kukabidhi mali za Jukwaa na taarifa zote kwa uongozi uliopo

#### 4.0.3.3 Kusitishwa kwa Uongozi wa Jukwaa;

Uongozi mzima wa Jukwaa unaweza kuondolewa pale ambapo: -

(i) Itakapothibitika kuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(ii) Wanachama wakipiga kura ya kutokuwa na imani, kwa zaidi ya asilimia hamsini na;

(iii) Ikibainika wanaendesha Jukwaa kwa maslahi binafsi.

**Tanbihi:** Viongozi waliositishwa kuongoza watawajibika kukabidhi mali na taarifa sahihi kwa wajumbe/wanachama (au viongozi wengine waliochaguliwa).

### 4.1 Uendeshaji wa Jukwaa

Viongozi waliochaguliwa katika kila ngazi watakuwa ndio kamati Tendaji ya Jukwaa, hivyo watahusika kusimamia shughuli zote za Jukwaa kwa ngazi husika, Aidha jukwaa linaweza kuwa na kamati za muda pale inapolazimu.

### 4.2 Mikutano ya Jukwaa

Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi litakuwa likiendeshwa kupitia mikutano mbalimbali kuanzia ngazi ya Mtaa/Kijiji hadi Mkoa. Aidha, uendeshaji wa Mikutano hiyo utakuwa kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Jukwaa la Mtaa/Kijiji

Mkutano wa wanachama wa jukwaa utaitishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa ngazi ya Mtaa/Kijiji husika na utafanyika mara nne kwa mwaka. Mkutano huu utakapoitishwa pamoja na mambo mengine utawajibika na yafuatayo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya jukwaa, zikiwemo fursa na changamoto;

(b) Kuweka mipango na mikakati ya utekelezaji wa maendeleo ya jukwaa;

(c) Kupokea na kujadili taarifa ya Fedha ya Jukwaa;

(d) Katika mwaka wa tatu wa kipindi cha uongozi na pale itakapohitajika kutakuwa na ajenda ya uchaguzi wa viongozi;

(e) Kupokea taarifa ya vikundi hai na vilivyojiunga na jukwaa.

**Tanbihi:** Ratiba ya Vikao hivi ifuatane na ratiba za vikao vya kisheria vya Mtaa/Kijiji ili taarifa za Jukwaa zijumuishwe kwenye vikao vya kisheria kama Vikao vya Maendeleo la Kijiji/Mtaa.

#### 4.2.2 Jukwaa ngazi la Kata

Mkutano wa wanachama wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ngazi ya Kata utaitishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo na utafanyika mara mbili kwa mwaka. Aidha Mwenyekiti anaweza kuitisha vikao vingine viwili vya dharula kulingana na mahitaji ya jukwaa la kata.

Wajumbe wa mkutano huu ni viongozi waliochaguliwa kutoka kwenye Mtaa/Vijii ambao ni: Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti, Katibu, Katibu

Msaidizi na Mweka hazina pamoja na wajumbe 5 waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Jukwaa la Kata. Mkutano huu utakapoitishwa pamoja na mambo mengine utafanya yafuatayo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya jukwaa, zikiwemo fursa na changamoto;

(b) Kuweka mikakati ya utekelezaji wa maendeleo ya jukwaa;

(c) Katika mwaka wa tatu wa kipindi cha uongozi na pale itakapohitajika kutakuwa na ajenda ya uchaguzi wa viongozi.

**Tanbihi:** Ratiba ya Vikao hivi ifuatane na ratiba za vikao vya kisheria vya kata ili taarifa za Jukwaa zijumuishwe kwenye vikao vya kisheria kama Baraza la Maendeleo la Kata (WDC).

### 4.2.3 Jukwaa ngazi la Wilaya

Mkutano wa wanachama wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ngazi ya Wilaya utaitishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo na utafanyika mara mbili kwa mwaka. Aidha Mwenyekiti anaweza kuitisha vikao vingine viwili vya dharula kulingana na mahitaji ya jukwaa la Wilaya. Wajumbe wa mkutano huu ni viongozi waliochaguliwa kutoka kwenye Kata ambao ni:

Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti, Katibu na Katibu Msaidizi pamoja na wajumbe 3 waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Jukwaa la Halmashauri. Mkutano huu utakapoitishwa pamoja na mambo mengine utafanya yafuatayo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya jukwaa, zikiwemo fursa na changamoto;

(b) Kuweka mipango na mikakati ya utekelezaji wa maendeleo ya jukwaa;

(c) Katika mwaka wa tatu wa kipindi cha uongozi na pale itakapohitajika kutakuwa na ajenda ya uchaguzi wa viongozi.

**Tanbihi:** Ratiba ya Vikao hivi ifuatane na ratiba za vikao vya kisheria vya kiutendaji vya Wilaya ili taarifa za Jukwaa zijumuishwe kwenye vikao vya kisheria kama kamati za huduma za Jamii, Fedha utawala na Mipango, Baraza la Maendeleo la Wilaya (DCC) na Baraza la Madiwani.

### 4.2.4 Jukwaa ngazi la Mkoa

Mkutano wa wanachama wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake

Kiuchumi ngazi ya Mkoa utaitishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo na utafanyika mara mbili kwa mwaka. Aidha Mwenyekiti anaweza kuitisha vikao vingine viwili vya dharula kulingana na mahitaji ya jukwaa la Mkoa. Wajumbe wa mkutano huu ni viongozi waliochaguliwa kutoka kwenye Wilaya ambao ni: Mwenyekiti na Katibu pamoja na wajumbe 2 waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Jukwaa la Wilaya kukiwa na uwakilishi wa wajumbe kutoka kila Halmashauri kama Wilaya itakuwa na Halmashauri zaidi ya moja. Mkutano huu utakapoitishwa pamoja na mambo mengine utafanya yafuatayo:

a) Kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya jukwaa, zikiwemo fursa na changamoto;

b) Kuweka mipango na mikakati ya utekelezaji wa maendeleo ya jukwaa;

c) Katika mwaka wa tatu wa kipindi cha uongozi na pale itakapohitajika kutakuwa na ajenda ya uchaguzi wa viongozi.

**Tanbihi:** Ratiba ya Vikao hivi ifuatane na ratiba za vikao vya kisheria vya kiutendaji vya Mkoa ili taarifa za Jukwaa zijumuishwe kwenye vikao vya kisheria kama Baraza la Maendeleo la Mkoa (RCC) na vikao vingine.

## SURA YA TANO

### 5.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU

Majukumu ya Wadau muhimu wanaohusika na uratibu, usimamizi na uendeshaji wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yameainishwa ili kutoa urahisi wa utekelezaji. Wadau hao ni;

1. Ofisi ya Rais – Ikulu;
2. OR TAMISEMI;
3. OR – Mipango na Uwekezaji;
4. OWM;
5. Wizara ya Fedha;
6. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;
7. Wizara za Kisekta;
8. Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
9. Sekretarieti za Mikoa;
10. Mamlaka za Serikali za Mitaa;
11. Asasi za Kiraia;
12. Sekta Binafsi na
13. Wadau wa maendeleo.

### 5.0 Ofisi ya Rais - Ikulu

Kwa kuwa majukwaa haya yalianzishwa na kuasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi hii itakuwa na **majukumu yafutayo**:

(i) Kutoa mwelekeo/dira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Jukwaa;
(ii) Kupokea taarifa ya utendaji wa Jukwaa kila baada ya miezi sita. Mlezi Mkuu wa majukwaa haya.

### 5.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI

Ofisi ya Rais - TAMISEMI itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kusimamia uanzishaji na **uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi** ya Mikoa na mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(ii) Kutoa maelekezo ya uteuzi wa Afisa Maendeleo ya Jamii kwa jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Jukwaa katika ngazi

za Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji / Mtaa;

(iii) Kupokea, kuchambua na kuandaa taarifa ya pamoja na kuiwasilisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;

(iv) Kusimamia utengaji wa bajeti, uanzishaji, uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya Jukwaa katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Kuweka Kasma ya utekelezaji wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi);

(v) Kuratibu na kuwaunganisha wadau wa maendeleo na Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Jukwaa;

(vi) Kujenga uelewa kwa jamii kuhusu Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(vii) Kusimamia utoaji wa mikopo 4% kwa wanawake inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri (10%);

(viii) Kuelekeza Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya Mikoa na Halmashauri kusimamia uchaguzi wa Viongozi wa Jukwaa la uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

### 5.2 OR –Mipango na Uwezeshaji

Wizara hii itakuwa na majukumu yafutayo:

(i) Kutengeneza Mipango na Mikakati ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi;

(ii) Kutengeneza na kuunganisha fursa za masoko kwa Jukwaa;

(iii) Kwa kushirikina na Wizara za Kisekta kutafuta fursa za kiuchumi mfano upatikanaji wa fedha, ujenzi wa viwanda n.k.

(iv) Kuingiza mipango ya uwezeshaji wanawake katika Mipango ya Nchi;

(v) Kuipa kipaumbele Mipango ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

### 5.3 Ofisi ya Waziri Mkuu

Ofisi hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Uratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

(ii) Kutoa Miongozo na maelekezo kwenye Wizara za Kisekta kuhusiana na Jukwa;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwenye majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi;

(iv) Itasimamia Kamati ya Uongozi.

### 5.4 Wizara ya Fedha

Wizara hii itakuwa na majukumu yafutayo:

(i) Kuandaa na kutoa miongozo ya Mipango na Bajeti kwa Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uwezeshaji wa Wanawake;
(ii) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Miongozo ya Mipango na Bajeti na;
(iii) Kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa.

### 5.5 Kamati ya Uongozi

Itaongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na itahusisha viongozi wakuu wa Wizara za uratibu, Wizara za Kisekta, Sekretariati ya kitaifa na Wadau kutoka Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wadau wa Maendeleo.

(i) Kupokea taarifa kutoka kwenye Sekretariati;
(ii) Kutoa ushauri wa uboreshaji wa Programu za Jukwaa;
(iii) Kuidhinisha mipango mipya na mikakati inayoletwa na Sekretariati.

### 5.6 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kubuni mikakati mbalimbali ya kuwainua wanawake kiuchumi kwa lengo la matokeo endelevu;
(ii) Kufanya mapitio ya Mwongozo;
(iii) Utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Jukwaa kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya Uwezeshaji Wanawake;
(iv) Kuwajengea uwezo waratibu wa Majukwaa katika ngazi zote;
(v) Kuratibu ushiriki wa wadau na hasa Asasi za Kiraia;
(vi) Kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata, Mitaa/Vijiji kwa kushirikiana na OR TAMISEMI;
(vii) Kufuatilia na kuratibu uimarishaji wa Jukwaa;
(viii) Kujenga uwezo wa viongozi wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi katika ngazi zote;
(ix) Kutoa elimu za uwezeshaji na uhamasishaji wa uundwaji wa

Jukwaa;

(x) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa;

(xi) Kufanya ufuatiliaji wa Pamoja (Joint Monitoring Visits) kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau;

(xii) Kujenga uelewa kwa jamii kuhusu Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(xiii) Kupokea taarifa ya kila robo mwaka kutoka OR-TAMISEMI;

(xiv) Utafutaji wa Rasilimali kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(xv) Kuwaunganisha wanawake na fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund – WDF) na ;

(xvi) Kusimamia uteuzi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwa Waratibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi zote.

## 5.7 Wizara za Kisekta

Wizara hizi kupitia Taasisi zake zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa watekelezaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi (mnyororo wa thamani);

(ii) Kuratibu upatikanaji wa mitaji kwa wanawake/ wanajukwaa

(iii) Kuunganisha jukwaa na fursa mbalimbali za kiuchumi kama vile masoko, teknolojia wezeshi na urasimishaji wa biashara.

(iv) Kushauri Jukwaa mbinu bora za kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

(v) Kutumia Jukwaa kama daraja la kutekeleza Programu zao mbalimnbali.

## 5.8 Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)

Baraza kupitia sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itafanya uratibu na Usimamizi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Maeneo yafuatayo:

(i) Kutengeneza Mikakati na Mipango ya upatikanaji wa fursa kwa Jukwaa

(ii) Kusimamia Programu za Uwezeshaji kwenye Jukwaa

(iii) Kubuni fursa kwa ajili ya Jukwaa.

(iv) Kufanya utambuzi na kutoa Tuzo kwa Mikoa iliyofanya vizuri

kwenye Jukwaa kwa ajili ya utambuzi.

(v) Kwa kushirikiana na WMJJWM Kujadili mafanikio na changamoto za Jukwaa na kushauri maboresho.

### 5.9 Sekretarieti

Sekretarieti itahusisha WMJJWM, OR-TAMISEMI na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Majukumu ya Sekretariati yatakuwa yafuatayo:

(i) Usimamizi na uratibu wa shughuli za Jukwaa.
(ii) Kuratibu vikao vya Wizara za Kisekta
(iii) Ufuatiliaji na Tathmini na kuweka mikakati
(iv) Kuhakikisha Mwongozo unatekelezwa ipasavyo.
(v) Kuandaa taarifa ya Jukwaa na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Uongozi.
(vi) Kutunza kumbukumbu za mikutano ya Kamati ya Uongozi kwa ajili ya Jukwaa.
(vii) Kuratibu vikao vya Kamati ya Uongozi

### 5.10 Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Majukumu ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya: -

(i) Watakuwa walezi wa Jukwaa katika maeneo yao ya utawala
(ii) Wasimamizi wakuu wa utekelezaji wa Jukwaa
(iii) Watakuwa ngazi ya rufaa ya masuala yote atakayowasilishwa kwao yenye viashiria vya migogoro inayohusiana na utendaji na utekelezaji wa shughuli za jukwaa.

#### 5.10.1 Sekretariati za Mikoa

Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuteua Afisa Maendeleo ya Jamii atakayeratibu na kusimamia shughuli za Jukwaa katika ngazi ya Mkoa
(ii) Kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.
(iii) Kusimamia mikutano ya jukwaa la uwezeshaji wanawake la Mkoa
(iv) Kupokea taarifa za utendaji wa jukwaa katika ngazi ya Wilaya, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja ya Mkoa na kuziwasilisha OR TAMISEMI.
(v) Kuwezesha upatikanaji wa jengo la Ofisi na ukumbi wa

kufanyika mikutano na makongamano ikiwemo jumba la maendeleo.

(vi) Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa la Mkoa.

(vii) Kutafuta vyanzo vingine vya fedha za kuwezesha uendeshaji wa Jukwaa.

(viii) Kusimamia uchaguzi wa Viongozi wa Jukwaa la Mkoa

### 5.10.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka hizi kwa maana ya Wilaya zikijumuisha (Halmashauri, Miji, Miji Midogo na Majiji) zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuteua Afisa Maendeleo ya Jamii atakayeratibu na kusimamia shughuli za Jukwaa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kata

(ii) Kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi ya kata, mtaa/kijiji

(iii) Kusimamia mikutano ya jukwaa la uwezeshaji wanawake katika ngazi ya Wilaya kila baada ya miezi sita katika mwaka wa fedha na pale itakapotokea mikutano ya dharula,

(iv) Kupokea taarifa za utendaji wa jukwaa katika ngazi ya Kata na Mtaa/Kijiji, kuzichambua, kuandaa taarifa za pamoja na kuziwasilisha ngazi ya Mkoa,

(v) Kuwezesha upatikanaji wa Ofisi na ukumbi wa kufanyia mikutano na makongamano ikiwemo jumba la maendeleo.

(vi) Kusimamia Uchaguzi wa Viongozi wa Jukwaa la Wilaya.

(vii) Kutenga maeneo ya kufanyia biashara na maonesho ya wajasiriamali,

(viii) Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa la Wilaya kwa Wilaya zenye Halmashauri zaidi ya moja bajeti zitaainishwa kwa kila Halmashauri husika na kuingizwa kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri (MTEF) ,

(ix) Kuwaunganisha wanawake na fursa za kiuchumi hasa mitaji, masoko, mikopo ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri

(x) Kutafuta vyanzo vingine vya fedha za kuwezesha uendeshaji wa Jukwaa.

### 5.13 Ofisi ya Kata

Ofisi ya kata itakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo: -

i. Kuratibu na kusimamia shughuli zote za Jukwaa (Afisa Maendeleo ya Jamii kata
ii. Kupokea, kusimamia na kutekeleza miongozo mbalimbali ya majukumu ya jukwaa kutoka ngazi ya Wilaya
iii. Kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi ya kata, Kusimamia mikutano ya jukwaa la uwezeshaji wanawake katika ngazi ya Kata,
iv. Kupokea taarifa za utendaji wa jukwaa katika ngazi ya mitaa/viijiji, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja na kuziwasilisha ngazi ya Wilaya,
v. Kuwezesha upatikanaji wa Ofisi na ukumbi wa kufanyikia mikutano na makongamano ikiwemo jumba la maendeleo,
vi. Kutenga maeneo ya kufanyia biashara na maonesho ya wajasiriamali,
vii. Kubaini vipaumbele vya mahitaji ya Jukwaa na kuviwasilisha kwenye Halmashauri ili kutengewa bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa,
viii. Kuwaunganisha wanawake na fursa za kiuchumi hasa mitaji, masoko, mikopo ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri
ix. Kutafuta vyanzo vingine vya fedha za kuwezesha uendeshaji wa Jukwaa.
x. Kusimamia \uchaguzi wa Viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi la Kata

## 5.14 Ofisi ya Mtaa/ Kijiji

Ofisi hii kupitia Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kupokea, kusimamia na kutekeleza miongozo mbalimbali ya majukumu ya jukwaa kutoka ngazi ya Kata,

(ii) Kuitisha mkutano wa wanawake wote kwa ajili ya kuwajengea wanawake uelewa kuhusu dhana ya Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi.,

(iii) Kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa Jukwaa katika ngazi ya Mtaa/Kijiji,

(iv) Kupokea taarifa za utendaji wa jukwaa kutoka kwa viongozi wa jukwaa ngazi ya mitaa/viijiji, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja na kuziwasilisha ngazi ya kata,

(v) Kuwezesha upatikanaji wa Ofisi na ukumbi wa kufanyikia mikutano na makongamano ikiwemo jumba la maendeleo,

(vi) Kwa kushirikiana na uongozi wa Mtaa/Kijiji kutenga maeneo ya kufanyia biashara na maonesho ya wajasiriamali,

(vii) Kubaini vipaumbele vya mahitaji ya Jukwaa na kuviwasilisha kwenye kata ili kutengewa bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa.

(viii) Kuwaunganisha wanawake na fursa za kiuchumi hasa mitaji, masoko, mikopo ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

(ix) Kusimamia uchaguzi wa Viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi la Kijiji, na

(x) Kuendelea kuhamasisha wanawake kuunda vikundi, kujisajili na kujiunga kwenye jukwaa.

# SURA YA SITA

## 6.0 UTARATIBU WA KUGHARAMIA SHUGHULI ZA JUKWAA

Mwongozo umezingatia umuhimu wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli za jukwaa ikiwemo kutafuta vyanzo vya mapato ya uendeshaji wa Jukwaa. Wizara ya Fedha itaingiza masuala ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Mwongozo wa Bajeti ya Serikali. Vivyo hivyo Wizara zote za Kisekta, Mikoa na Halmashauri zitawajibika kuingiza Mipango na Bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Jukwaa kwa kila Mwaka.

Katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Jukwaa, Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya (Kijiji/Mtaa, Kata, Halmashauri, Mkoa na Wizara) wataandaa bajeti ya shughuli za Jukwaa kuiwasilisha kwa Wakuu wa ngazi husika kwa ajili ya kuunganishwa kwenye Mpango na Bajeti wa Mwaka.

### 6.0 Vyanzo Vya Mapato ya Jukwaa

Utekelezaji wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi utafanyika kwa kutegemea Miradi na Bajeti za Wizara za Kisekta, vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri, Ruzuku ya uendeshaji wa Ofisi (OC), Harambee, ufadhili kutoka Taasisi za fedha na nyinginezo, Asasi za Kiraia, Wadau wa Maendeleo na watu binafsi watakaokubali kuchangia shughuli za jukwaa kwa ngazi husika.

### 6.1 Matumizi ya fedha za Jukwaa

Matumizi ya fedha ya Jukwaa ambayo yamepatikana kutoka Serikalini au chanzo kingine ikiwemo wadau yatatumika kwa mujibu wa malengo yake na Mratibu atatoa taarifa ya matumizi. Matumizi ya fedha zote za Jukwaa yatazingatia mipango, taratibu na miongozo ya fedha za Serikali. Ikumbukwe akaunti pekee ya jukwaa itamilikiwa na jukwaa la kijiji ambako kuna vikundi. Hii haiondoi /haifuti utaratibu wa vikundi kuwa na akaunti za uendeshaji wa shughuli za kikundi.

# SURA YA SABA

## 7.0 UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Ufuatiliaji na tathmini wa Jukwaa umejumuisha taratibu za uendeshaji Jukwaa na utoaji wa taarifa za utekelezaji. Sekretarieti itakuwa na wajibu wa kutoa miongozo na vigezo vya ubora wa taarifa, aina za taarifa, muda wa kutoa taarifa na mtiririko wa utoaji wa taarifa za Jukwaa.

### 7.1. **Ufuatiliaji**

Sekretarieti ya Jukwaa itakuwa na dhamana ya kufanya ufuatiliaji shirikishi wa utekelezaji wa shughuli za Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. (Kiambatisho Na. 2 Vigezo vya Ufuatiliaji na Tathimini Mikoa na Wilaya) Aidha, Vigezo vitakavyozingatiwa kupima utekelezaji wa mwongozo ni vifuatavyo:-

(i) Uundaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata na Mitaa/Vijiji.

(ii) Uimarishaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata na Mitaa/Vijiji.

(iii) Mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa Jukwaa (wajumbe),

(iv) Mafunzo ya kuwajengea uwezo Waratibu, wajumbe, wajasiriamali na wanawake,

(v) Utengaji na upatikanaji wa fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya Jukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi,

(vi) Jumla ya mikopo iliyotolewa kutoka kwa wadau na idadi ya wanawake walionufaika,

(vii) Miundombinu iliyowekwa katika Mikoa au Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha shughuli za majukwaa.

(viii) Ajira zilizozalishwa katika uanzishaji na uendeshaji wa Jukwaa,

(ix) Idadi ya maonesho ya biashara yaliyofanyika na Idadi ya wanawake walioshiriki maonesho hayo,

(x) Takwimu za matukio ya kazi zilizotekelezwa na Jukwaa katika ngazi mbalimbali, na

(xi) Uwepo wa mifumo ya mawasiliano

(xii) Kiasi cha mikopo iliyotolewa kutoka kwenye taasisi za fedha, wadau na idadi ya wanawake walionufaika

***Tanbihi:* Vigezo vingine vitatongezeka kulingana mahitaji**

## 7.2 Tathmini

Tathmini ya Jukwaa italenga kuona Kama jukwaa limesaidia kubadilisha hali ya uchumi wa mwanamke. Aidha, tathmini itaongeza wigo, ubora na ufanisi wa jukwaa la wanawake na shughuli zilizofanyika. Hii itajumuisha huduma zinazotolewa na wadau wa kisekta. Tathmini hii itafanyika kila baada ya miaka mitatu ,itahusisha kuingia mikataba ya utekelezaji ,uratibu na uendeshaji wa shughuli za Jukwaa ili kusimamia ufanisi na ufasaha na itaangalia viashiria vifuatavyo:

(i) Idadi ya wanawake waliokopeshwa na fursa walizounganishwa nazo,

(ii) Idadi ya viwanda vilivyoanzishwa,

(iii) Ajira zilizotengenezwa,

(iv) Shughuli ndogo ndogo za kiuchumi zilizoanzishwa,

(v) Idadi ya wanawake waliowezeshwa kupata teknolojia rahisi na sahihi, na aina ya teknolojia za uzalishaji.

(vi) Idadi ya shughuli za ujasiriamali za wanawake zilizofanyika hususani biashara ndogo, kilimo, madini, usafirishaji, usindikaji, uhunzi n.k zilizonufaika,

(vii) Idadi ya biashara ndogo zilizounganishwa na taasisi au huduma za kifedha (mikopo),

(viii) Idadi ya mikutano ya Jukwaa iliyofanyika,

(ix) Idadi ya wanawake waliohudhuria katika mikutano iliyoandaliwa,

(x) Idadi ya wanawake walioshiriki matukio ya uwezeshaji, mf. Maonesho.

(xi) Idadi ya biashara za wanawake zilizorasimishwa,

***Tanbihi:* Vigezo vya tathimini vinaweza kuongezeka kulingana mahitaji**

### 7.3 **Utoaji wa Taarifa za utekelezaji**

Kila Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, zihakikishe zinafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi katika maeneo yao na kutoa taarifa kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI / WMJJWM. Katika kufanikisha majukumu ya utekelezaji wa Jukwaa, kila Sekretatieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kupanga na kutenga bajeti ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Jukwaa. Ufuatiliaji, utoaji wa taarifa na tathmini uzingatie utekelezaji wa kila jukwaa lililoainishwa kwenye ngazi husika ya utawala kama ilivyooneshwa katika Mwongozo huu. Ufuatiliaji na tathmini utaonesha vigezo vya ubora wa taarifa zikiwemo taarifa za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na taarifa ya mwaka. Masuala mengine yatakayozingatiwa ni muda wa kutoa taarifa na mtiririko wa taarifa.

Aidha, itaandaliwa mikataba ya ufuatiliaji wa utekelezaji pamoja na kutoa tuzo ya kila mwaka kwa ngazi iliyofanya vizuri. Utaratibu utawekwa wa kiongozi wa juu kusaini Mkataba huo. Viongozi wa Mikoa nao watasaini mikataba ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa jukwaa na viongozi walio chini yao.

# SURA YA NANE

## 8.0 HITIMISHO

Mwongozo huu ni muhimu katika kuelekeza watendaji na wadau wa utekelezaji wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kuwa na uelewa wa pamoja wa namna bora ya kuunda na kuhuisha Jukwaa. Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali watasimamia uundaji wa Jukwaa na upatikanaji wa viongozi watakaopewa dhamana

ya kuongoza Jukwaa katika sehemu husika. Kila mdau wa Mwongozo huu anawajibika kuuelewa bayana na kuufanyia kazi ipasavyo kulingana na wajibu na majukumu aliyonayo katika utekelezaji wa Jukwaa.

Mwongozo huu utakuwa zana ya kuboresha muundo, uendeshaji na ufuatiliaji na tathmini kwa Jukwaa na hivyo kuwa kielelezo cha hatua zinazotakiwa kufuatwa katika uundaji na uratibu wa Jukwaa kwa upande wa Tanzania Bara. Mwongozo hautaathiri utendaji kazi wa mifumo iliyopo ya Serikali bali utasaidia kuiwezesha kutoa huduma kwa walengwa kwa maslahi ya mwanamke wa kipato cha chini na Taifa kwa ujumla.

Katika kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo huu, Jukwaa la Mkoa na Wilaya litaandaa Mpango mkakati wa utekelezaji.

**JEDWALI NA.1 Rejista ya Uandikishaji wa vikundi vilivyojiunga na Jukwaa Halmashauri ya ……………………………………………….**

| Halmashauri | Kata | Mtaa/Kijiji | Jina la Kikundi | Idadi ya Wanachama | Shughuli za Kikundi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

**JEDWALI NA.2 Mpango kazi wa utekelezaji wa shughuli za Jukwaa ngazi ya……………………………**

| Na | Lengo | Lengo Mahsusi | Kiashiria | Shabaha | Shughuli | Muda | Rasilimali Zinazohitajika | Mashirikiano/ Washirika | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |